

HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO

(Barua zote za kiofisi zitumwe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji (W))

Simu: 027-2552225

Fax: 027-2555679

E-Mail ded@simanjirodc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)
S.L.P. 9596,

ORKESUMET -SIMANJIRO

Kumb.Na. HMW/SMJ/SB.10/05/125

05.10.2020

TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Kufuatia tangazo la ajira lenye Kumb.Na. HMW/SMJ/B/VOL.I/15/55 la tarehe 7.09.2020 lililohusu nafasi mbili (2) ya Mtendaji wa Kijiji daraja III (1) na Katibu Mahususi daraja III (1) Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Simanjiro inawatangazia waombaji waliokidhi vigezo kufika kwenye usaili.

1. Usaili utafanyika tarehe 15.10.2020 saa 2:30 asubuhi katika Ukumbi wa Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro.
2. Wasailiwa wote wanatakiwa kufika na vyeti halisi (Orginal Certificates) vya taaluma, mafunzo ya ujuzi, cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha NIDA au Kitambulisho cha mpiga kura au barua ya utambulisho kutoka kwa Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa anakoishi mhusika.
3. Aidha atakayekuja na "transcript" "result slip" pekee bila vyeti halisi hataruhusiwa kufanya usaili.
4. Waombaji waliosoma nje ya nchi wahakikishe wanakuja na uthibitisho kutoka TCU na NACTE.
5. Waombaji ambao hawajaona majina yao hawajakidhi vigezo hivyo wanashauriwa kuomba tena nafasi zikitangazwa.
6. Katika zoezi hili Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya ya Simanjiro haitahusika na gharama zozote za waombaji katika kipindi chote cha usaili (usafiri, chakula na malazi)

Pamoja na Tangazo hili, orodha ya majina ya wasailiwa imeambatishwa hapa chini.


Yefred Myenzi

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SIMANJIRO

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SIMANJIRO

